
# MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA, 2022) KWA MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

**Imetolewa: (02/09/2022)**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa msimu wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba -Disemba, 2022; athari na ushauri kwa sekta mbalimbali katika mkoa wa Kaskazini na wilaya zake:

**(I) Ngazi ya Mkoa**




**Kielelezo 1: (a)** Mwelekeo wa msimu wa Vuli, 2022 kwa kisiwa cha Unguja. (b) Ramani inayoonesha wastani wa muda mrefu wa mvua za msimu wa Vuli katika sehemu mbalimbali za kisiwa cha Unguja. **Angalizo**: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za mwezi Oktoba hadi Disemba, mabadiliko ya mvua kati ya mwaka mmoja na mwingine yamezingatiwa.

**Dondoo**

- *Kwa ujumla mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya mkoa wa Kaskazini Unguja.*
- *Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya nne ya mwezi Oktoba na wiki ya kwanza ya mwezi Novemba, 2022.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha mwezi Januari, 2023.*
- *Vipindi virefu vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi vinatarajiwa katika msimu huu wa Vuli.*


**Mvua za msimu wa Vuli, 2022**

Kwa ujumla mvua zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi ya wilaya za Mkoa wa Kaskazini Unguja. Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya nne ya mwezi Oktoba na wiki ya kwanza ya mwezi Novemba, 2022.

***Angalizo:***
*Ingawa maeneo mengi yanatarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani, izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza yakajitokeza katika maeneo machache.*

# MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA, 2022) KWA WILAYA YA KASKAZINI 'A', UNGUJA
## Umetolewa: 02/09/2022

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba-Disemba, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Kaskazini 'A', Unguja.




Mwelekeo wa mvua za Vuli Oktoba -Disemba, 2022 kwa wilaya ya Kaskazini 'A', Unguja.

## Dondoo muhimu

- *Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya Wilaya ya Kaskazini 'A'.*
- *Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya nne ya mwezi Oktoba na wiki ya kwanza ya mwezi Novemba, 2022.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha mwezi Januari,2023.*
- *Wakulima na wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji na uzalishaji wa mazao ili kukabiliana na upungufu wa mvua.*

## Mvua za msimu wa Vuli, 2022 kwa wilaya ya Kaskazini 'A'.

**Zitaanza:** Kati ya wiki ya nne ya mwezi Oktoba na wiki ya kwanza ya mwezi Novemba, 2022.

**Zitaisha:** Januari, 2023.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa chini ya wastani hadi wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Oktoba -Disemba kwa Wilaya ya Kaskazini 'A' ni kati ya milimita 190 hadi 200.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Disemba, 2022.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano wa kutokea vipindi virefu vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Vuli, 2022.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko hafifu katika maeneo mengi ukilinganisha na Vuli iliyopita.

## Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**

- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

## Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

### Matokeo

- Upungufu wa unyevunyevu katika udongo katika maeneo mengi unaweza kuathiri uzalishaji wa mazao ya chakula, biashara na matunda yakiwemo mpunga, migomba, mahindi, mtama, karafuu, nazi, michungwa na mishoki shoki.
- Magonjwa ya mifugo na wadudu waharibifu wa mazao hasa wakati wa msimu wa mvua yanaweza kujitokeza.
- Upungufu wa mvua unaweza kuathiri upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo.
- Uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya baharini unatarajiwa kupungua.

### Ushauri

- Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora za muda mfupi zinazoendana na urefu wa msimu.
- Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua.
- Wafugaji wanashauriwa kufuata njia bora za ufugaji ikiwemo kupanda malisho na uhifadhi.

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: **www.meteo.go.tz**



*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Morogoro Rd, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3,
S.L.P. 3056, Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8.
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz


**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA, 2022) KWA WILAYA YA KASKAZINI'B', UNGUJA
## Umetolewa: 02/09/2022

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba-Disemba, 2022; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Kaskazini 'B', Unguja.




Mwelekeo wa mvua za Vuli Oktoba -Disemba, 2022 kwa wilaya ya Kaskazini 'B', Unguja.

### Dondoo muhimu

- *Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Kaskazini 'B'.*
- *Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya nne ya mwezi Oktoba na wiki ya kwanza ya mwezi Novemba, 2022.*
- *Mvua zinatarajiwa kuisha mwezi Januari,2023.*
- *Wakulima na wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji na uzalishaji wa mazao ili kukabiliana na upungufu wa mvua.*

### Mvua za msimu wa Vuli, 2022 kwa wilaya ya Kaskazini 'B'.

**Zitaanza:** Kati ya wiki ya nne ya mwezi Oktoba na wiki ya kwanza ya mwezi Novemba, 2022.

**Zitaisha:** Januari, 2023.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa chini ya wastani hadi wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Oktoba -Disemba kwa Wilaya ya Kaskazini 'B' ni kati ya milimita 190 hadi 195.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Disemba, 2022.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano wa kutokea vipindi virefu vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Vuli, 2022.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko hafifu katika maeneo mengi ukilinganisha na Vuli iliyopita.

### Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**
- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

**Matokeo**

- Upungufu wa unyevunyevu katika udongo katika maeneo mengi unaweza kuathiri uzalishaji wa mazao ya chakula, biashara na matunda yakiwemo mpunga, migomba, mahindi, mtama, karafuu, nazi, michungwa na mishoki shoki.
- Magonjwa ya mifugo na wadudu waharibifu wa mazao hasa wakati wa msimu wa mvua yanaweza kujitokeza.
- Upungufu wa mvua unaweza kuathiri upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo.
- Uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya baharini unatarajiwa kupungua.

**Ushauri**

- Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora za muda mfupi zinazoendana na urefu wa msimu.
- Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua.
- Wafugaji wanashauriwa kufuata njia bora za ufugaji ikiwemo kupanda malisho na uhifadhi.

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: **www.meteo.go.tz**


*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Morogoro Rd, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3,
S.L.P. 3056, Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8.
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz


**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**



**Taarifa hii Imetolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania**